

Kutafuta mahali pa kupanga kunachukua muda. Kuna mambo mengi ya kufikiria na kujifunza, hasa kama wewe ni mpangaji wa mara ya kwanza.

Wakati unapokodi nyumba katika NSW unakuwa mpangaji.

Nchini Australia wapangaji wana haki na majukumu.

Kufahamu haki zako na majukumu yako kabla kupanga kutasaidia kutatua matatizo yoyote kati ya kabaila yako, ajenti wa mali isiyohamishika, wapangaji wenzako au majirani yako.

Jambo la kwanza kufikiria unapotafuta mahali pa kuishi ni kiasi gani unachoweza kulipa kwa kodi.

Kuna aina nyingi ya miliki ya kuchagua.

Unahitaji tu kuchagua aina nzuri zaidi ya miliki inayofaa kwako na familia yako.

Nyumba na bustani yake, nyumba ya mjini au vyumba vinavyoweza kuwa karibu zaidi usafiri.

Fikiria kuhusu safari kwenda kazini, maduka, mashule na vituo vya daktari.

Inabidhi ufikirie pia kuhusu eneo unapotaka kuishi. Maeneo mengine yana miliki ya kupanga ya bei chini zaidi.

Gharama ya kodi itategemea aina ya miliki unayotaka kupanga, na maeneo unakotaka kuishi.

Itabidhi ulipe kodi kila wiki au kila wiki mbili.

Kwa hiyo, angalia kipato chako na budgeti kufahamu kiasi unachoweza kulipa kwa kodi – baada ya kununua chakula na bidhaa nyingine na mahitaji mengine ya kuishi.

Majimbo tofauti nchini Australia yana masheria tofauti kuhusu kupanga.

Biashara ya Haki inatoa maelezo ya upangaji na msaada kwa wapangaji, makabaila na maajenti katika NSW. Pia ni shiriko la serikali linalotunza dhamana ya kodi na kusimamisha Maajenti wa Mali Isiyohamishika katika NSW.

Kupata maelezo zaidi kuhusu haki na majukumu ya wapangaji, tembelea tovuti ya www.fairtrading.nsw.gov.au au piga simu namba ya 13 32 20.

Kama ukihitaji msaada wa lugha pigia simu 13 14 50.

Kwa hiyo yupo tayari kupanga nyumbani yako?